



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

TANGAZO KWA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI (NGOs)

Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali anayatangazia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) kuwasilisha taarifa zao za mwaka 2021 na kulipa ada kuanzia tarehe **01 Januari, 2022**. Ada ya mwaka ni Shilingi 50,000/= kwa Mashirika ya Ndani (Local NGOs) na USD 100 kwa Mashirika ya Kimataifa (International NGOs). Mwisho wa kuwasilisha taarifa na kulipa ada ya mwaka 2021 ni tarehe **15 Aprili, 2022** saa **9:30 Alasiri**. Baada ya tarehe hiyo malipo yote ya ada yatalipwa na faini ya Tshs.100,000/= kwa Mashirika ya Ndani na USD 300 kwa Mashirika ya Kimataifa.

Taarifa hizo ziwasilishwe kupitia mfumo wa usajili wa NGOs **nis.jamii.go.tz** kwa kutumia Akaunti za Mashirika. Aidha, kwa wale wasio na Akaunti hizo waombe kupitia **www.jamii.go.tz** katika kipengele cha **NGOs MIS** na kisha kujaza fomu kiufasaha na kuiwasilisha.

Hakutatolewa muda wa ziada wa kuwasilisha taarifa, na kutowasilisha taarifa ni kinyume na kifungu cha 29(1) (a) na (b) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na.24 ya mwaka 2002 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2005 na 2019.

Vickness G. Mayao

MSAJILI WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

Tel: 0737 569 583/ 0737 569 584

29 Disemba, 2021
